Je, vituo vya afya vipo kwa manufaa ya wananchi?

Wananchi na wafanyakazi katika vituo vya afya wazungumzia huduma

1. Utangulizi

Kutibu watu wanapougua kunahitaji mfumo unaoeleweka wenye kutoa ugunduzi wa ugonjwa, ushauri, huduma na utoaji dawa. Tanzania inao mfumo huu ila unakibiliwa na changamoto nyingi, ikiwapo uhaba wa wafanyakazi. Wananchi hukabiliana na changamoto hizi kila siku. Watu watatu kati ya watano hawaridhiki nayo. Asilimia 41 ya wananchi walisema kuwa Serikali inashughulikia uimarishaji wa huduma za msingi za afya kwa udhaifu mkubwa sana; na asilimia 22 walisema kuwa Serikali inaishughulikia suala hili kwa udhaifu mkubwa. Ni asilimia 6 tu ya wananchi ndio wanaosema kuwa Serikali inashughulikia jambo hili vizuri sana; na asilimia 28 walisema Serikali inajitahidi kiasi chake. Je, nini kimejificha ndani ya taarifa hizi? Muhtasari huu unaonyesha matokeo mapya kuhusu utoaji huduma za afya nchini Tanzania, ukionyesha takwimu za hivi karibuni kuhusu mada hii.

Matokeo haya yanatokana na awamu ya nne ya utafiti wa *Sauti za Wananchi*, ambao ni wa kwanza wa aina yake barani Afrika wenye kutumia simu ya mkononi kukusanya maoni yenye uwakilishi wa nchi nzima. (www.twaweza.org/sauti). Takwimu zilikusanywa kutokana na jopo la wahojiwa waliokuwa wakitokea nchini kote Tanzania Bara. Simu zilipigwa kati ya tarehe 17 Juni na tarehe 3 Julai; takwimu zilijumuisha majibu kutoka kwenye kaya 1,722 na vituo vya afya 92. Takwimu pia zilijumuisha maoni ya wahojiwa ambao walishiriki kwenye jaribio la ufuatiliaji na usimamiaji uliofanyika katika vituo vya afya 132 na maduka ya dawa 61. Muhtasari huu vile vile unawasilisha matokeo ya utafiti wa msingi wa *Sauti za Wananchi* ambao ulifanyika kati ya Oktoba 2012 na Januari 2013.

Muhtasari huu umeandikwa na kutayarishwa na Twaweza, iliyopo Hivos Tanzania.
Imetolewa Novemba 2013

S.L.P. 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 266 4301 Nukushi: +255 22 266 4308.
Baruapepe: uwazi@twaweza.org Tovuti: www.twaweza.org/sauti

Twaweza ni sisi

Utafiti huo uliendeshwa miongoni mwa kaya 1,679 (mahojiano kwa simu) na vituo vya afya 114 (kwa kutembelea vituo vya afya).

Matokeo muhimu ya muhtasari huu ni:

- Asilimia 77 ya wagonjwa huenda kwenye hospitali za serikali
- Zahanati ya kawaida zina asilimia 50 tu ya wafanyakazi wanaotakiwa kuwapo
- Asilimia 32 ya wagonjwa husubiri kwa zaidi ya saa moja kabla ya kuhudumiwa
- Tiba kwa watoto wa chini ya umri wa miaka mitano kwa kawaida si bure

2. Mambo saba kuhusu huduma za afya nchini Tanzania

Jambo la 1: Watanzania hutegemea vituo vya afya vya serikali

Zaidi ya nusu (57%) ya Watanzania walipata huduma kwenye vituo vya afya kati ya Mei na Juni, 2013, aidha kupata tiba au kumsindikiza mgonjwa. Idadi kubwa ya waliokwenda hospitali (77%) walikwenda kwenye vituo vya afya vya Serikali (kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo cha 1). Vituo vya afya vya binafsi na vya madhehebu ya dini vinachangia kiwango kidogo tu katika kutoa huduma za afya.

Kielelezo cha 1: Je, ulikwenda kwenye kituo cha aina gani cha afya?



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi:*
Utafiti kwa kutumia Simu ya Mkononi, Awamu ya 4, Juni 2013.

Jambo la 2: Katika maeneo ya vijijini, asilimia 37 ya wagonjwa hutembea mwendo wa saa nzima au zaidi kupata huduma ya afya

Umbali wa kituo cha afya ni kigezo cha muhimu kinachowafanya wagonjwa waamue ni wakati gani katika hatua ya kuugua kwao waanze kutafuta tiba. Katika hali ngumu zaidi, hili huwa ni suala la kufa na kupona. Kama inavyoonyeshwa kwenye Kielelezo cha 2, wagonjwa wengi vijijini na mijini hutumia hadi dakika 30 kufika kituoni wakihitaji

huduma za afya. Hata hivyo, mara nyingine safari hii inaweza ikawa ndefu zaidi: vijijini, asilimia 27 ya watu hutumia saa nzima; na asilimia 10 hutumia saa mbili kufika katika kituo cha afya.

Kielelezo cha 2: Muda wanaotumia kufika katika kituo cha afya



Chanzo cha takwimu: wa *Sauti za Wananchi:*
Utafiti kwa kutumia Simu ya Mkononi, Awamu ya 4, Juni 2013.

Jambo la 3: Vituo vya afya vinaajiri wafanyakazi wachache sana

Matatizo nchini Tanzania katika kuajiri na kuwabakisha katika ajira wafanyakazi wa kutosha katika sekta ya afya yameshaandikiwa kwa kiasi kikubwa. [1] Je, hali iko vipi hivi sasa katika vituo vya afya? Kielelezo cha 3 kinaonyesha viwango vya ajira vya wafanyakazi wa sekta ya afya wakati wa kufanya utafiti wa msingi wa *Sauti za Wananchi* (2012) kwa kutembelea zahanati (D) na vituo vya afya (HC).[2] Viwango vilivyopendekezwa vimenukuliwa kutoka katika chapisho la Manzi na wenzake. (2012).[3] Matokeo kwa kiasi kikubwa yanaoana na upungufu wa wafanyakazi uliokwishaonekana tangu hapo awali: zahanati ya kawaida ina asilimia 50 tu ya idadi inayopendekezwa, kwa upande wa utabibu na huduma za uuguzi. Vituo vya afya navyo vile vile vina upungufu wa wafanyakazi kwa maana ya manesi, lakini vyenyewe vina nafuu kidogo kwa upande wa wafanyakazi wa utabibu.

1 Mwaka 2007, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (MoHSW) ilieleza kwamba: "Kwa mujibu wa viwango vya wafanyakazi wa MoHSW (1999), wataalamu wa afya waliofuzu wapatao 46,868, wanahitajika katika vituo vya afya vya umma. , Wataalamu waliopo ni 15,060 ambao ni sawa na asilimia 32.1% ya mahitaji. Hii ina maana kuna upungufu wa wafanyakazi 31,808 sawa na asilimia 67.9." (Primary Health Services Development Programme, MMAM 2007 – 2017, page 10).

2 Kwa kuwa kuna hospitali chache tu katika sampuli, hatujumuishi kipengele hiki.

3 Manzi et al.: Human resources for health care delivery in Tanzania: a multifaceted problem. Human Resources for Health 2012 10:3. Clinical staff includes Medical Doctors, Assistant Medical Officers and (Assistant) Clinical Officers.

Kielelezo cha 3: Wafanyakazi walioajiriwa katika sekta ya afya



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi*,
Utafiti wa Msingi wa Vituo vya Afya, Oktoba - Desemba 2012 & Manzi na wenzake

Jambo la 4: Asilimia 31 ya wafanyakazi katika vituo vya afya hawafiki kazini

Moja ya kiashiria kilichotumika sana kubaini ubora wa huduma za afya ni wafanyakazi kutokuwepo kazini, jambo lililodhihirika vituo vilipotembelewa kwa kushtukiza. Iwapo wafanyakazi katika sekta ya afya ni watoro mara nyingi, wananchi hulazimika kubaki pasipo huduma au hupaswa kusubiri kwa muda mrefu sana. Jambo hili linapunguza ari/nia yao ya kutafuta huduma hii muhimu. Kielelezo cha 4 kinaonyesha kiwango cha utoro kwa wafanyakazi katika vituo vya afya vya vijijini (ikijumuisha watabibu, manesi, wafanyakazi wa maabara, wafanyakazi katika kitengo cha utoaji dawa, wahudumu na wafanyakazi wengine), ambao ni asilimia 31 kwa wastani. . Kiwango cha utoro kinabaki pale pale iwapo watabibu wanapopambanuliwa – ingawa watabibu katika vituo vya afya vya mijini wana uwezekano mkubwa zaidi wa kuwepo kazini (asilimia 29 ya utoro, haijaonyeshwa) kuliko wafanyakazi wengine (35%).

Kielelezo cha 4: Viwango vya utoro wa wafanyakazi katika sekta ya afya



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi*,
Utafiti wa Msingi wa Vituo vya Afya, Oktoba - Desemba 2012.

Jambo la 5: Asilimia 32 ya wagonjwa husubiri kwa zaidi ya saa nzima kabla ya kuhudumiwa

Baada ya mgonjwa kufika katika kituo cha afya, je, humpasa kusubiri muda gani kabla ya kuhudumiwa na mfanyakazi wa kituo? Kielelezo cha 5 kinaonyesha kuwa zaidi ya nusu (55%) ya wagonjwa wanaokwenda vituo vya afya husubiri kwa muda usiozidi nusu saa. Wagonjwa walio wengi wanaokwenda kwenye vituo vya afya vya serikali husubiri kwa zaidi ya nusu saa kabla ya kumwonana mfanyakazi wa kituo cha afya.

Kielelezo cha 5: Muda wa kusubiri katika kituo cha afya



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi:*
Utafiti kwa kutumia Simu ya Mkononi, Awamu ya 4, Juni 2013.

Jambo la 6: Wagonjwa hushawishika zaidi kutoa rushwa katika vituo vya afya vya serikali

Upungufu wa wafanyakazi na muda wa kusubiri huwaweka katika hali ngumu wafanyakazi na wagonjwa pia. Je, wagonjwa hutoa rushwa katika vituo vya afya ili wahudumiwe haraka? *Sauti za Wananchi* iliwauliza wahojiwa kama walitoa rushwa mara ya mwisho walipokwenda kwenye kituo cha afya; Asilimia 5% ya wahojiwa walisema ndiyo. (Kumbuka kwamba hili ni suali nyeti kwa hiyo ni muhimu kuchukulia majibu haya kwa tahadhari). Kilelelezo cha 6 kinaonyesha kuwa mgonjwa anayekwenda kwenye kituo cha afya cha serikali ana kishawishi mara mbili zaidi cha kutoa rushwa kulinganisha na mgonjwa anayekwenda kwenye kituo cha afya cha binafsi.

Kielelezo cha 6: Je, ulilazimika kutoa rushwa katika kituo cha afya?



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi:*
Utafiti kwa kutumia Simu ya Mkononi, Awamu ya 4, Juni 2013.

Jambo la 7: Kwa kawaida watoto hawapewi huduma bure

Watoto walio na umri chini ya miaka 5 na watu wazima wenye umri zaidi ya miaka 60 wanatakiwa kupata huduma bure kwenye kituo cha afya cha serikali, iwapo hajalazwa. Mahojiano na kaya yanaonyesha kwamba, walipokwenda kutibiwa kituo cha afya mara ya mwisho, watoto ndio waliopata huduma za bure mara nyingi zaidi kuliko watu wazima wenye umri wa miaka 60 na zaidi – ingawa huduma ya bure ni nadra. Ni katika asilimia 18 tu ya watoto wanaomwona daktari ambao wazazi wao wanasema hawakutoa fedha zozote. Yaani, hata kwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano, matibabu yao kwa kawaida huhitaji kaya itoe fedha (ikiwa ni pamoja na kwa kumwona daktari, kupata dawa au kufanyiwa vipimo).

Kielelezo cha 7: Kaya zinazopata huduma ya bure kwa watu wazima kuanzia miaka 60 na watoto wenye umri chini ya miaka 5



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi,*
Utafiti wa Msingi wa Vituo vya Afya, Oktoba - Desemba 2012.

3. Hitimisho

Muhtasari huu unatoa ripoti kuhusu changamoto zinazowakabili wagonjwa na wafanyakazi katika mfumo wa huduma za afya. Wahojiwa katika utafiti huu wa *Sauti za Wananchi* na wafanyakazi wa vituo vya afya katika jamii walieleza vikwazo walivyokuwa wakikumbana navyo vikiwemo: wagonjwa kulazimika kwenda mwendo mrefu ili kufikia kituo cha afya; vituo vya afya kuwa na upungufu wa wafanyakazi – jambo linalowafanya wagonjwa wasubiri kwa muda mrefu; na pia kuwepo kwa tuhuma za rushwa. Matatizo haya, pamoja na mengineyo yanaweza kusababisha wagonjwa kuacha kuonana na wataalamu wa afya kwa ajili ya ushauri na kupata dawa.

Afya ya taifa inategemea kwanza: ubora na idadi ya wafanyakazi wake, pamoja na upatikanaji wa dawa na vifaa vya tiba. Vyote hivi mwishowe hutegemea upatikanaji wa rasilimali kwa kila mmoja kwa ajili ya huduma za afya kwa wote.

Wananchi wenye afya bora zaidi, kwa wastani, ndio wenye kuzalisha zaidi – hivyo basi, mara kwa mara hutokea kuwa ndiyo wenye utajiri wa kumudu huduma bora za afya. Kwa maneno mengine, utajiri wa taifa huwa unapelekea kiasi cha, na ubora wa huduma za afya ambayo taifa itamudu kutoa kwa wananchi wake. nazoweza kumudu. Hata hivyo, rasilimali siyo kigezo pekee. Ubora wa huduma za afya hutegemea pia usahihi na ufanisi ambao rasilimali hizi hutumiwa, hasa katika muktadha wa mfumo ulio mkubwa na uliotawanyika kama uliopo Tanzania.

Katika miaka ya hivi karibuni, Tanzania imepiga hatua kubwa katika kujenga vituo vya afya. Lakini, je, vituo hivi vinawahudumia watu? Matokeo yaliyowasilishwa kupitia muhtasari huu yanaibua masuala muhimu matatu. Kwanza, je, kiasi cha bajeti kinachotengwa kwa ajili ya sekta ya afya katika ngazi ya juu kinatosha? Pili, je, wafanyakazi, pamoja na fedha na bidhaa vinafika pasipo kupotea au kucheleweshwa? Rasilimali zisizopatikana ipasavyo zinahitaji kutumiwa kwa uangalifu, na ni muhimu kushughulikia mahitaji yanayojotokeza na kulenga kuleta suluhisho zenye ufanisi. Mafunzo kwa wafanyakazi wa afya na maslahi yao katika kazi ni suala muhimu mno. Suala la tatu na la mwisho ni hamasa kwa wafanyakazi: hata pale nafasi zote zinapojazwa na akiba ya dawa ikiwapo ya kutosha, mfumo utaweza tu kutoa huduma bora pale wafanyakazi wanaposaidiwa na kupewa hamasa ya kuwepo kazini na kutoa huduma bora.